



## Sera ya kupinga ubaguzi wa rangi

Wapendwa wazazi na walezi,

Idara ya Elimu inakataa aina zote za ubaguzi wa rangi na imejitolea kukomesha aina zote za ubaguzi wa rangi katika shule za umma za NSW. [Anti-Racism Policy](#) (Sera ya Kupinga Ubaguzi wa Rangi) ya Idara inalenga kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi, mfunyakazi, mlezi, au mwanajamii anayekumbana na ubaguzi wa rangi katika mazingira ya shule.

Sera ile huomba watu wote wa jamii ya shule kusaidia katika kukabiliana na ubaguzi wa rangi kwa kuonyesha heshima kwa asili ya kitamaduni, kiisimu na kidini ya wengine, na kwa kuishi kwa njia zinazokuza kukubalika na maelewano katika mazingira ya shule.

Kila shule ina Afisa wa Mawasiliano wa Kupinga Ubaguzi wa Rangi (Anti-Racism Contact Officer (ARCO)) ambaye amefunzwa kusaidia na kukabiliana na ubaguzi wa rangi na kuunga mkono na jamii ya shule inapofanya malalamiko ya ubaguzi wa rangi katika shule. Kwa maelezo zaidi kuhusu sera ile na kazi ya ARCO angalia [Anti-Racism Policy - Information for parents and carers](#) (Sera ya Kupinga Ubaguzi wa Rangi – Maelezo kwa wazazi na walezi).

Asante kutusaidia kuendeleza mazingira mazuri ya shule ambamo aina zote za ubaguzi wa rangi zinakataliwa. Tafadhali wasiliana nami ikiwa wewe au mtoto wako unapata aina yoyote ya ubaguzi wa rangi, unashuhudia mtu yeyote akikabiliwa na ubaguzi wa rangi katika shule yetu, au ungetaka maelezo au msaada zaidi.

Wako mwaminifu

Mwalimu mkuu

## Msaada wa mkalimani

Ikiwa ungetaka maelezo zaidi na unahitaji mkalimani kukusaidia kuwasiliana na shule au Mwalimu mkuu tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na omba mkalimani katika lugha yako.

Umwambie opereta wa simu nambari ya simu ya shule na opereta atapigia simu shule na kupata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo yako.

Hutatozwa kwa huduma za ukalimani.